MADA YA SAIKOLOJIA

SABABU ZA KISAKOLOJIA ZINAZOFANYA WATU WASIWEKE AKIBA WALA KUWEKEZA KWA MANUFAA YAO YA BAADAYE

Imewasilishwa na;

HAPPINESS MILINGA

Daktari wa Saikolojia & Ushauri

Kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar

19.09.2026 Dodoma, Tanzania

YALIYOMO

1. UTANGULIZI
2. KUHIFADHI PESA MAANA YAKE NI NINI
3. PESA INA KAZI GANI KISAIKOLOJIA
4. SABABU ZA KISAKOLOJIA ZA KUTOWEKA AKIBA NA KUWEKEZA
5. KWA NINI WATU HUUMIA SANA WAKIPOTEZA HELA
6. NINI KIFANYIKE ILI KUWEKA AKIBA
7. HITIMISHO

UTANGULIZI

- **Kwa nini watu hawahifadhi pesa? Wanaogopa nini?**
- **Ni nini kinachosukuma watu kutumia pesa zote tu bila kuwekeza kabisa?**

Maswali hayo Pamoja na mengine yatajibiwa katika mada hii.

Aidha,maamuzi yetu ya kifedha huathiriwa na mambo mengi ikiwemo mambo kama:

- Saikolojia ya Fedha Nyingi. Saikolojia ya Fedha kidogo.
- Maumivu ya moyo au ubongo yatokanayo na kupoteza Fedha.
- Ukosefu wa Maarifa ya masuala ya Fedha, n.k.

Na mwishoni Kila mmoja atapata tiba ya Kisaikolojia kuhusu Fedha na mafanikio yanayojengwa juu ya saikolojia ya mafanikio.

Kuhifadhi (Saving) Pesa Kuna Maana Gani?

- ✓**Ni kuweka pesa benki na kutozigusa kwa muda fulani.**
- ✓**Ni kuweka pesa kwenye biashara ili ziongezeke kupitia faida.**
- ✓**Ni kununua mali ambayo thamani yake huongezeka kwa muda Fulani .**
- ✓**Kumpatia ndugu akutunzie kwa woga wa kuzitumia vibaya**
- ✓**Kusaidia watu ili na yeye aje asaidiwe baadaye.**
- ✓**Kutoa sadaka kwenye Nyumba za Ibada**

Pesa Ina Kazi Gani Kisaikolojia?

Katika Mtazamo wa Kisaikolojia, Pesa ina kazi zifuatazo

1. **Huleta raha na furaha kwa mwenye nayo**
2. **Kuhisi uko salama muda wote**
3. **Kuwa na Heshima mtaani au katika jamii**
4. **Mamlaka na Uwezo**
5. **Amani ya Moyo**
6. **Hauna sonona (Stress)**

SABABU 6 ZA KISAIKOLOJIA ZA KUTOWEKA AKIBA NA KUWEKEZA



1. Kujilinganisha Na Wengine – (Social Comparison)

Hali ya kujipima thamani na watu wengine kwenye mafanikio na hata furaha yake

Inapelekea kutokuwekeza kwa sababu;

- ✓Tunafanya ununuzi wa kujionyesha (kulingishia wengine mafanikio yako)
- ✓Hisia ya kuchelewa kufanikiwa. (Unajiona kama umechelewa maishani)
- ✓Matumizi ya kufuata mkumbo. Kwenda bar, kununua gari, simu kali, kusomesha Watoto shule kali, vipodozi, saluni, n.k).

UBONGO WETU HAUNA KIPIMO CHA NDANI KWAMBA MIMI NI SAWA BALI UNATUMIA WENGINE KAMA RULA(Watu ambao mko hali moja)

2. Kutaka kupata raha mara moja (Instant gratification)

- Ni msukumo wa ubongo wa mtu hupenda kuwa na hali ya raha muda wote au papo hapo
- Ubongo hutoa dopamine(kemikali ya furaha)
- Kuchukia shida na mateso na kwa kutaka kufanya vitu vinavyoridhisha ubongo kwa haraka kama kulala mda wote,kutumia mitandao ya Kijamii

Madhara yake;

- Inapunguza nidhamu binafsi kwenya matumizi ya pesa
- Hupunguza uvumilivu

3.Imani Kwamba Akiba Lazima Iwe Kubwa Ili Iwe na Maana

Kuamini kuwa kiasi kidogo cha hela haikina thamani kubwa kwenye uwekezaji hii inatokana na;

✓Kujilanganisha na wenngine

✓Ubongo kuona kitu kidogo hakiwezi kutoa matokeo makubwa

✓**Kukosa Elimu ya compound interest. (Faida limbikizi, dundulizi,)**


Mfano; *“hii 10,000/= yangu ni ndogo sana ngoja nipate pesa kubwa ndio nianze kuwekeza*”

“ Haba na haba hujaza kibaba”


NMB
Karibu yako

4. Kukosa uvumilivu na hofu ya kupoteza pesa

- Uwekezaji unahitaji uvumilivu wa mda mrefu ili kupata faida. Tulio wengi hatuna uvumilivu kwenye mambo ya Fedha kwa sababu kesho(future) yetu tunaiona mbali.
- Tuna hofu ya kupoteza Fedha kwa uoga wa kuanza upya.
- Pia inatokana na kutokua na Imani na tasisi za kifedha kama bank, kampuni za uwekezaji na serikali



Takwimu za Hali ya Kuziamini Benki na Mitandao ya Simu (MNO)

5. Mirorongo Mirefu ya Uwekezaji

- Taasisi Nyingi hutumia utaratibu mrefu wa kuweka akiba au Kuwekeza
- Watu hulazimishwa kuwasilisha nyaraka Nyingi
- Maelezo yanakuwa mengi na kukatisha tamaa

KWA KUWA UBONGO HAUPENDI MIRORONGO MINGI:

1. Huamua kuachana na baishara hiyo au uwekezaji huo
2. Hutafuta njia nyepesi na rahisi mbadala wa hiyo ngumu

6. Msukumo wa Kijamii Kutumia Fedha (The Social Pressure to Spend)

Ni Msukumo Kutoka kwa jamii, familia, marafiki, wageni unaokufanya uhisi ulazima wa kutumia pesa, Ili usionekane mchoyo au maskini.

Ubongo wetu una hofu ya asili ya kukataliwa au kutengwa

KWA NINI WATU HUUMIA SANA KISAIKOLOJIA WAKIPOTEZA

1. **Ubongo huona Hasara kama tishio. Maumivu ya kupoteza huwa makubwa kuliko furaha kupata Fedha**
2. **kujiambatanisha kihisia na Fedha zetu**
3. **Kuogopa majuto(regret) baada ya Kupata Hasara (“nilisema mimi”)**
4. **Kuthamini tulichonacho kuliko tunachoweza kupata baadaye**
5. **Hasara ya Sasa hivi huonekana Kubwa kuliko Faida ya Baadaye**
6. **Aibu ya Kijamii na Kuchekwa au Kukushangaa sana.**
7. **Tishio kwa utambulisho wako mbele za Watu Uliowaheshimu. Kuhisi kushuka kwa heshima na hadhi yako.**

NINI KIFANYIKE ILI KUWEKEZA FEDHA KWA FAIDA YA BAADAYE

1. Tambua kuwa Maisha yana dharura Nyingi zinazotusubiri
2. Tambua kuwa ubongo wetu una uwezo wakujirekebisha(neuroplasticity)
3. Tenga asilimia ndogo ndiyo uiweke akiba na nyingine kula bata
4. Chunguza faida unayoipata badala ya Hasara unayoiwaza kutokea
5. Wekeza Fedha ambayo ikipotea Haikumii (Money yo can afford to lose)
6. Tambua kuwa Maisha yamejaa Kuanguka na Kuinuka. kuanguka ndiyo kufanikiwa kwenyewe FADEMO
7. Usijiambatanishe na Mali yako (Get detached from Money).
8. Anza kuweka kidogo kidogo ili kujenga tabia endelevu ya kuwekeza
9. Anza na Mpango wa Akiba ya Dharura kujikinga na Majanga.
10. Usijilanganishe na wengine. Ishi maisha yako.

Hitimisho

- ✓Tujenge tabia endelevu ya kuweka akiba bila kusubiri kupewa motisha
- ✓Umaskini hautafutika kwako kama utaendelea kutumia pesa zako zote
- ✓Matajiri watabaki kuwa Matajiri kwa sababu wao huwekeza kwanza kabla ya kufanya matumizi yoyote,
- ✓Maisha yamejaa Changamoto Nyingi, Ukiogopa kupoteza hautapata mafanikio kamwe.
- ✓Ubongo wako lazima uuzoeze kujifunza kuhusu Fedha, akiba na uwekezaji ndipo baada ya muda utazoea kuweka akiba na kuwekeza

ASANTE KWA KUNISIKILIZA

KARIBUNI SANA KWA;

MASWALI NA MAJADILIANO